OMAHA Public Schools

district.ops.org

# Habari ya Mwanafunzi

| Jina la Ukoo la Mwanafunzi: |
|---|
| Jina la Kwanza la Mwanafunzi: |
| Darasa / Nambari ya kitambulisho cha Mwanafunzi |

## Jukumu la Mzazi/ Mlezi katika matumizi ya Teknolojia

Shule za Umma za Omaha zinaweza peana kwa mwanafunzi wako kifaa cha teknolojia kwa mwaka wa shule 2021-2022. Kama mzazi au mlezi halali wa mwanafunzi, lazima ukiri kutumia matumizi ya teknolojia yaliyotajwa hapa chini. Ili kuonyesha kwamba umesoma na kuelewa jukumu la mzazi au mlezi katika matumizi ya teknolojia, **tafadhali sahihisha kisanduku kilichoko hapa chini**.

☐ **Sheria:** Wanafunzi wanaweza kutumia kifaa cha teknolojia cha Shule za Umma za Omaha mwaka wa shule wakiwa wamesajiliwa. Endapo usajili wa mwanafunzi utakamilika, mzazi au mlezi arudishe kifaa cha teknolojia anapoamuriwa chini ya wiki mbili baada ya kuamuriwa, kikiwa kwa hali salama kama vile kilivyokua alipopewa. Kukosa kurudisha kifaa hicho cha teknolojia, kutapelekea mzazi au mlezi kulipa Shule za Umma za Omaha gharama yote ya hicho kifaa, na pia gharama ya wakili na gharama zingine zitakazo tokana na kufuatilia kifaa hicho. Shule za Umma za Omaha pia zinahifadhi haki ya kukatiza umiliki ikiwa mzazi au mlezi, au mwanafunzi anaaminika kuwa amekiuka sehemu yoyote ya haya Makubaliano ya Matumizi ya Teknolojia, Matumizi Sahihi ya Mwanafunzi na Mwongozo wa Usalama wa Mtandao, au Kanuni za Maadili ya Mwanafunzi.

☐ **Umiliki:** Kifaa cha teknolojia ni mali inayomilikiwa kipekee na Shule za Umma za Omaha. Hamna wakati wowote umiliki utahamishwa kwa Mzazi/Mlezi au mwanafunzi.

☐ **Ubadilishaji wa anuani:** Kifaa cha teknolojia kitabakia katika anuani aliyotoa mwanafunzi katika fomu ya usajili. Taarifa iliyoandikwa lazima itolewe katika Shule za Umma za Omaha katika siku 30 ikiwa anuani hiyo itabadilika.

☐ **Masharti:** Mzazi/Mlezi anakubali kuripoti hasara au uharibifu utakaotokea kwa kifaa cha teknolojia chini ya siku 3 baada ya hasara au uharibifu kutokea. Mzazi/ Mlezi atamuarifu mwalimu kupitia barua pepe. Mzazi/Mlezi atawajibikia kipekee kwa uharibifu au hasara itakayo fanyikia kifaa hichi cha teknolojia. Ikiwa kifaa cha teknolojia kitaripotiwa kuharibika au kuibwa shuleni, shule itashirikiana na afisa wa usalama au afisa rasilimali wa shule kufaili ripoti ya polisi.

☐ **Udumishaji na Urekebishaji:** Mzazi/Mlezi au mwanafunzi ana jukuma la kuomba udumishaji na urekebishaji wa kifaa cha teknolojia akiwa amekimiliki. Mzazi/Mlezi au mwanafunzi atajulisha wafanyakazi wa shule hitaji la kurekebisha kifaa cha teknolojia.

☐ **Matumizi ya teknolojia:** Mzazi/Mlezi anakubaliana na yafuatayo:

1) Kifaa cha teknolojia kitatumika kwa masomo ya mwanafunzi aliyesajiliwa katika Shule za Umma za Omaha na sio kwa faida ya mtu mwingine au kwa kusudi lengine lolote.
2) Kila programu iliyotolewa itakua chini ya, na itumike kulingana na leseni na/au makubaliano yanayotokana na iyo programu.
3) Matumizi yote ya kifaa cha teknolojia yatakua chini ya sera na sheria za Shule za Umma za Omaha zinazohusiana na matumizi ya mtandao. (rejelea kitabu cha mwongozo)
4) Mzazi/mlezi peke yake ana jukumu la kuhakikisha kwamba mipangilio ya programu, usanidi chaguo-msingi na haki za usimamizi hazibadilishwi au kugeuzwa kutoka kwa mpangilio asili kifaa kilikuwa nayo kilipopokelewa.
5) Mzazi/Mlezi na mwanafunzi kwa pamoja wana jukumu la kuweka utatumbulisho na nywila za matumizi kwa usiri kuzuia matumizi yasiyoruhusiwa.

## Mpango wa Kinga ya Hiari ya Kifaa

**Mzazi/Mlezi anawajibu kwa upotevu, wizi ama uharibifu wa kifaa.** Wilaya imeanzisha Mpango wa Kinga ya Hiari ya Kifaa. Mzazi/mlezi anaweza sajiliwa kwenye Mpango wa Kinga ya Hiari ya Kifaa kwa mwaka wa shule 2021-2022 **kwa kulipa malipo ya mara moja, kwa mwaka ya $20 kwa kila kifaa.** Mzazi/Mlezi yeyote anayekataa kushiriki kwa Mpango wa Kinga ya Hiari ya Kifaa anawajibika kwa bei halisi ya kubadilisha au kutengeneza kifaa kilichopotea, kilichoibiwa au kuharibika. **Kushiriki kwa hii Programu ni kwa Hiari**.

☐ **Mfuniko:** Kwa kushiriki kwa Mpango wa Kinga ya Hiari ya Kuchunga Kifaa, kipakatilishi au vifaa vingine vya eletroniki vitatengenezwa au kubadilishwa bila gharama kwa mzazi/mlezi, isipokuwa pale uharibifu au kupotea kwa kifaa umetokana na sababu ambazo zimeelezwa hapa chini:

- <u>Kupotea ambako Hakuelezeki au Kupotea kwa Ajabu:</u> Wilaya haiweza kufunika hasara iliyosababishwa na ukosaji wa kupata kifaa isipokua pale hali inaonyesha kuwa kifaa hicho kiliibiwa.
- Kukosa Kuwajulisha Polisi ikiwa Kifaa kiliibiwa: Ikiwa kifaa kiliibiwa, Mzazi/Mlinzi anafaa kuwajulisha polisi mara moja anapogundua kuwa kifaa kimeibiwa. Programu haitoi mfuniko ikiwa washiriki watakosa kuwajulisha polisi.

3) Matendo ya kimakusudi: Programu hii haitagharamia hasara inayotokana na uharibivu wa kusudi chini ya hii sera.
4) Vitendo vya udanganyifu: Programi hii haitagharamia hasara yeyote itakayotokana na udanganyifu au njia siziso halali.
5) Wizi kutoka kwa Gari Lisiloshughulikiwa: Programu haitagharamia hasara au uharibifu inayotokana na gari lisiloshughulikiwa isipokua pale ambapo gari limefungwa, madirisha yamefungwa na kuna ushahidi kuwa kuingia kwa hilo gari ulilazimishwa.
6) Kutengenezwa Ambako Hakuruhusiwi: Programu haitagharamia uharibifu ambao ulitokana na kijaribu kutengeneza au kutengenezwa na fundi asiyeidhinishwa na wilaya.
7) Kutoripoti kwa Muda Unaofaa: Programu yaweza kosa kugharamia kuharibika au hasara ambayo haikuripotiwa chini ya siku 3.
8) **Hakuna mfuniko unaotolewa kwa vifaa vya ziada: Programu haitagharamia vifaa kama kamba za umeme, vifaa vya ziada, begi, chaja, au vifaa vingine vya ziada.**

Wilaya itaamua ikiwa kifaa kilichoharibiwa kitatengenezwa au kitabadilishwa. Idara ya Bima ya Wafanyakazi na Ufadhili itaamua ikiwa hali ya kuharibika au hasara itagharamiwa kwenye programu na uamuzi wao ndio wa mwisho.

## Uchaguzi wa Mzazi/Mlezi Katika Mpango wa Kinga ya Hiari ya kifaa.

☐ Napiga kura kufuatia Mpango wa Kinga ya Hiari ya Kifaa:
Ndio nachagua kusajili mwanafunzi wangu kwa wilaya **kulinda kifaa kwa hiari. Nimejumuisha malipo ya $20.**

☐ La, nakataa kusajili mwanafunzi wangu kwa wilaya kulinda kifaa kwa hiari. Naelewa kuwa ninawajibika kwa malipo halisi ya ubadilishaji au kutengeneza kifaa cha teknolojia kilichopotea, kuibiwa au kuharibiwa wakati kifaa hakipo katika wilaya.

## Kukiri na sahihi ya Mzazi/Mlezi

Nimesoma na nimeelewa au nimeelezewa na nimeelewa wajibu wangu katika Uwajibu wa Utumiaji wa Teknolojia, Matumizi Sahihi ya Mwanafunzi na Mwongozo wa Usalama wa Mtandao, Kanuni za Maadili ya Mwanafunzi, na Mpango wa Kinga ya Hiari ya Kulinda kifaa. Nakubali kuzingatia na kuhakikisha kwamba mwanfunzi wangu anazingatia sheria na masharti yaliyotajwa kwenye Uwajibu wa Utumiaji wa Teknolojia, Matumizi Sahihi ya Mwanafunzi na Mwongozo wa Usalama wa Mtandao na Kanuni za Maadili ya Mwanafunzi na nakubali kupunguza matumizi ya hivi vifaa kwa matumizi ya masomo pekee. Nitaweza jititahidi kuhakikisha mwanafunzi wangu atazingatia sheria na masharti humu ndani. Nitampa ruhusa mwanangu kupata na kutumia teknolojia inayotolewa na Wilaya.

Shule za Umma za Omaha zitafanya kila juhudi kuzuia wanafunzi kupata taarifa zisizo za maadili mema kupitia kuendelea kutumia njia ya teknolojia ya ulinzi (kwa mfano kichujio cha wavuti) walakini naelewa kwamba haiwezekani kwa Wilaya kudhibiti na kuzuia utata au nyenzo zisizofaa ambazo zaweza kupatikana kutoka kwa vifaa vya Wilaya.

Wilaya haiwajibiki kwa hasara yeyote inayotokana na matumizi ya vifaa vya Wilaya na haitoi hakikisho lolote kwamba teknolojia ama mtandao wa Wilaya ambao unatumiwa na wanafunzi utapatikana kwa wakati wote.

Kwa kuweka sahihi nakubali kufuata masharti yaliyonakiliwa pale juu na kuchukua wajibu kuchunga na kutumia kwa umakini teknolojia inayotolewa na Wilaya. Naelewa kwamba ikiwa mimi au mwanafunzi wangu tutakosa kufuata masharti yote yaliyomo humu ndani, upatikanaji wa teknolojia, mtandao, na vyombo vya habari vya electroniki, unaweza kukataliwa katika siku zijazo. Zaidi, mwanafunzi wangu anaweza kuaadhibiwa kulingana na sheria za Kanuni za Maadili ya Shule za Umma za Omaha. Kwa hivo nashikilia bila hatia Shule za Umma za Omaha, maafisa wake, wanachama wa bodi, wafanyakazi na mawakala wake na wale wote wanahusianana Wilaya dhidi ya dhima, hasara, gharama au kudai kuumizwa kwa mwanafunzi kutakaotokana na matumizi ya kutumia vifaa vya teknolojia kwa mwanafunzi.

| Jina la Mzazi/Mlezi (tafadhali chapisha): | |
|---|---|
| Tarehe: | Sahihi ya Mzazi/Mlezi: |

district.ops.org

# Habari ya Mwanafunzi

| |
|---|
| Jina la Ukoo la Mwanafunzi: |
| Jina la Kwanza la Mwanafunzi: |
| Darasa / Nambari ya kitambulisho cha Mwanafunzi: |

## Matumizi Sahihi ya Mwanafunzi na Mwongozo wa Usalama wa Mtandao

Shule za Umma za Omaha zaweza kutoa na kupeana kibao au kipatakilishi kwa matumizi ya maelezo moja kwa moja na nyumbani kama njia ya kukuza mafanikio na kutoa urahisi wa fursa ya kusoma. Huu muongozo unatoa habari kuhusu matarajio ya Wilaya kwa wanafunzi na familia ambao wanapewa hizi vifaa vya electroniki. Kuongezea na huu Muongozo, matumizi ya teknolojia inayotolewa na Wilaya au mtandao pia inahitaji wanafunzi kufuata kanuni za mwenendo OPS Kanuni za Maadili ya Mwanafunzi, Kuongezea, muongozo zaidi unaweza kuongezwa pale inahitajika na itaongezwa humu ndani. Kuonyesha kwamba umesoma na kuelewa Matumizi Sahihi ya Mwanafunzi na Mwongozo wa Usalama wa Mtandao, tafadhali sahihisha kila sanduku lililoko hapa chini.

☐ **Majukumu ya Mwanafunzi:** Wanafunzi lazima kwa uwajibikaji watumie teknolojia ya Wilaya na waelewe vikamilifu utumiaji wa teknolojia na rasilimali ya wilaya. Wanafunzi lazima waweke vifaa ambavyo wamepewa na Wilaya salama na katika njia salama ili viweze kufanya kazi kwa njia inayostahili. Wanafunzi na familia watumie akili ya kawaida ili kujali na kutunza teknolojia waliyopewa na wilaya. Wanafunzi watafanya yafuatayo:

1) Kufuata haya maelezo na yale yaliyonakiliwa kwa Kitabu cha Mwongozo cha OPS na Kanuni ya Maadili ya Mwanafunzi kila wakati wanatumia vifaa vya teknolojia ndani ya shule na nje ya shule.

2) **Kuhakikisha kuwa vyombo vya teknolojia vina moto** ili kuhakikisha kwamba vinakuja shuleni vikiwa kama chaji imejaa ( darasani hamna uwezo kwa wanafunzi wote kuweka chaji vifaa hivi mchana)

3) Kuonyesha **uraia wa kidijitali chanya wakiwa mtandaoni**. Wanafunzi sharti watumie lugha iliyo njema katika mawasiliano yao yote wakiepuka matusi, uhayawani na matamshi ya kukera. Udhalishaji wa mtandaoni, ikiwemo shambulio la kibinafsi au vitisho dhidi ya mtu yeyote inayofanywa unapotumia teknolojia ya wilaya au teknolojia ya kibinafsi haikubaliki na inafaa iripotiwe kwa yule anayehusika shuleni.

4) Heshimu uchujaji kwa mtandao na kipimo cha usalama kinacho husishwa kwenye kipatakilishi au kibao. Kila kompyuta ya kila mwanafunzi imeundwa na yaliyomo kwenye mtandao wakati mwanafunzi yupo shuleni au wakati yupo katika mitandao ya umma au ile ya kibinafsi.

5) Chelezo faili za data zile ambazo ni muhimu kila wakati. Inapendekezwa kwamba wanafunzi kuweka **cheleza kwenye Wingu kutumia Office 365 OneDrive kama mahali pa kuweka cheleza**. OPS itasahihisha na kudumisha vifaa kwa kuzipiga picha mara kwa mara. Wanafunzi wataarifiwa kuhusu huku kudumishwa mapema. Kila faili cheleza ya kila mwanafunzi ambazo hazitakuwa zimekuwa cheleza kwenye nafasi ya hifadhi ya seva au hifadhi zingine za midia zaweza zikapotea wakati wa hiyo harakati. Ulizia msaada ikiwa hujui kuweka cheleza.
6) Tumia teknolojia kwa mambo yanayohusiana na shule pekee na epuka kutumia teknolojia kwa mambo ya kibiashara au kisiasa.
7) **Fuata sheria ya hatimiliki na miongozo ya matumizi ya haki** pakua tu au agiza muziki , video au yaliyomo ambayo wanafunzi wanaruhusiwa au ile halali inayokubaliwa kutoa au kutumika.
8) Tengeneza kwa ukaguzi na msimamizi mkuu au mwalimu taarifa zozote au faili zilotumwa au kupokelewa kutoka kwa mtandao wowote ukitumia teknolojia ya wilaya. **Wanafunzi wana notisi kwamba <u>hawana matarajio yeyote ya siri</u> katika kifaa kinacho milikiwa na Wilaya.** Faili na habari zinazopatikana, kupakuliwa au kuenezwa katika teknolojia ya wilaya zinaweza kuonekana,kufuatiliwa au kuhifadhiwa kwenye nyaraka wakati wowote.
9) Kumjulisha mwalimu wao au mkuu wa programu mara moja ikiwa tatizo la usalama limeonekana kwenye kompyuta za shule, mtandao au muunganisho wa intaneti.

☐ **Vizuizi vya wanafunzi:** Mwanafunzi **hafaai**:

1) **Kuweka alama, kupambua au kuweka stika ya plastiki kwenye** kipakitilishi, kibao au kesi zilizotolewa na wilaya.
2) Kuonyesha au kuchapisha taarifa za binafsi, faili au kuzungumza na watu usiowajua kupitia barua pepe au njia zingine kupitia kwenye mtandao.
3) **Kujaribu kughairi, kupita au kubadilisha kichujio mtandao** programu, jinsi kifaa kimeundwa au usanidi wa mtandao.
4) Kujaribu kufikia mtandao na teknolojia zingine bila ya idhini za kuingia. Hii inahusu pia **kutumia akaunti ya mtu mwingine, pia/au nywila** au kufikia mitandao iliyo madhubuti.
5) **Kugawa nywila au kujaribu kufumbua nywila.** Kugawa nywila hakuruhusiwi na inaweza fanya uadhibiwe na ushtakiwe kwa makosa ya watu wengine ikiwa shida itatokea kwa matumizi yasiyoruhusiwa.
6) **Kupakua na/au kuweka programu, faili au <u>michezo</u>** kutoka kwenye mtandao au vyanzo hadi kwenye teknolojia inayomilikiwa na Wilaya. Hii inahusu kukusudia kuleta virusi vya kompyuta na programu zingine kwa nia mbaya.
7) Badilisha vifaa vya programu , kujaribu kuingia kwenye kompyuta bila idhini, na/ **au kuharibu faili za kompyuta**. Kuharibu kwa makusudi au kwa uzembe kompyuta au programu za kompyuta yaweza pelekea mashtaka ya jinai.

8) Kujaribu kupata, kuona, kugawa au kuweka habari ambazo hazikubaliki shuleni. Hii inahusu ila sio tu ponografia, machukizo, vurugu za picha, au picha za matusi, sauti, lugha, video au habari zingine.
9) **Kukopesha kifaa chako au chaja na waya za kifaa na zingine.**
10) Kuacha kifaa kwenye gari au kukiacha bila kukiangalia wakati wowote.
11) Kula au kunywa wakati unatumia kifaa kwa ukaribu.
12) Kutumia au kukiwacha kifaa kwa maeneo hatari kama kwenye meza, sakafuni, kwenye kiti au kikiacha na wanyama-vipenzi.
13) **Kuweka vitu juu ya kifaa chako,** kukiacha inje au karibu na maji kama pale pa kuogelea.

## Kukiri na sahihi ya mwanafunzi.

Nimesoma na nimeelewa au nimesomewa na nimeelezwa Matumizi Sahihi ya Mwanafunzi na Mwongozo wa Usalama wa Mtandao na Kanunu za Maadili ya Mwanafunzi. Nakubali kufuata sheria na masharti yaliyonakiliwa kwenye Matumizi Sahihi ya Mwanafunzi na Mwongozo wa Usalama wa Mtandao, na Kanuni za Maadili ya Mwanafunzi na nakubali kutumia vifaa hivi kwa madhumuni ya masomo.

| | |
|---|---|
| Tarehe: | Sahihi ya mwanafunzi: |